

<INSERT DISTRICT OR SCHOOL INFORMATION & LOGO>

Ustahiki wa Mwanzo wa Usaidizi wa Ziada wa Lugha

SAMPULI YA BARUA YA TAARIFA YA MZAZI: Barua hii inatolewa na Idara ya Elimu ya New Hampshire kama aina ya Usaidizi wa Kiufundi kwa Mashirika ya Elimu ya Eneo (LEA) tunayosaidia. LEA zinaweza kuchagua kubinafsisha barua hii ili iendane na mipango ya eneo. Tunapendekeza sana kwamba LEA; ziweke tarehe ya barua, zipate saine, na zihifadhi nakala iliyotiwa saine katika faili ya jumla ya mwanafunzi.

Sampuli hii inajumuisha viwango vya chini zaidi vinavyohitajika chini ya *ESEA* §1112(e)(3) na (e)(4), 20 USC 6312 (2015) ili kukidhi masharti ya utifu kwa taarifa ya mzazi. Barua ya taarifa ya mzazi lazima itolewe kwa wazazi wa wanafunzi wote wa EL ndani ya siku 30 za kalenda mwanzoni mwa mwaka wa masomo au ndani ya siku 14 za kalenda baada ya mwanzo wa mwaka wa masomo.

Jina la Mwanafunzi: _____ Tarehe: _____
(mm/dd/yyyy)

Shule: _____ Gredi: _____

Mpendwa Mzazi au Mlezi:

Ulipomsajili mtoto wako shuleni uliombwa ujaze fomu ya Utafiti wa Lugha ya Nyumbani. Kwenye fomu hiyo ulisema kwamba lugha nyingine isipokuwa Kiingereza inazungumzwa nyumbani kwako. Kulingana na maelezo haya, shule ilimpa mtoto wako mtihani wa kupima Ufasaha wa Lugha ya Kiingereza (ELP) wa kimasomo. Madhumuni ya mtihani huo ni kubainisha kiwango cha ELP kwa wanafunzi wanaozungumza lugha nyingi ili kuhakikisha kuwa lugha si kizuizi katika kuelewa maudhui ya kimasomo ya kiwango cha gredi.

Tathmini ya ELP inayotumika katika New Hampshire ni Kichunguzi cha WIDA (WIDA Screener). Kama unavyojua, ukuzaji wa lugha ni mchakato unaoendelea kwa wote. Kichunguzi cha ELP hupima mahali mtoto wako yuko kwa sasa katika mchakato wa ukuzaji wa lugha ya Kiingereza.

Mtoto wako alipata alama ya jumla ya _____ kwenye kipimo cha 1-6. Unaweza kupata maelezo zaidi kwenye ripoti iliyoambatishwa ya alama.

1-Kuingia	2-Kuanzia	3-Kuendelea	4-Kupanuzi	5-Kuziba	6-Kufikia
-----------	-----------	-------------	------------	----------	-----------

Katika New Hampshire, mtoto yeyote anayepata alama za jumla za **4.4 au chini** anatambuliwa kama "mwanafunzi wa Kiingereza" (EL). Sheria ya shirikisho inahitaji shule za umma kutoa Mpango wa ziada wa Elimu ya Lugha ya Mafundisho (LIEP) au "mpango wa EL" kwa wanafunzi wote wanaostahiki huduma za lugha ya Kiingereza. Kulingana na matokeo ya mtoto wako ya mtihani wa ELP, **mtoto wako HASTAHIKI huduma hizi.**

Tafadhali weka barua hii kwenye rekodi zako. Katika siku zijazo, ukigundua mtoto wako anatatizika shuleni na unafikiri lugha inaweza kuwa ndio sababu, tafadhali wasiliana na shule kwa usaidizi. Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali wasiliana na mwalimu aliyeorodheshwa hapa chini.

<INSERT CONTACT INFORMATION>